**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO**

**ITHIBATI YA UBORA KIMATAIFA (ISO 9001:2015)**

# Orodha ya Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao

**Februari, 2025**

# 1. Muhtasari wa Miongozo ya Serikali Mtandao

## A. Miongozo ya Ngazi ya Sera – Ngazi ya 1

| Na | Jina la Nyaraka | Namba ya Nyaraka | Toleo/Mwaka |
|---|---|---|---|
| 1. | Mwongozo wa Serikali Mtandao | - | Desemba – 2017 |
| 2. | Mwongozo wa Usanifishaji Mpango wa Shughuli | eGA/EXT/AVS/004 | Ver 1.0 – Desemba 2024 |
| 3. | Mwongozo na Viwango vya Mfumo Jumuishi wa Kielektroni wa Usimamizi wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya | - | Nov 2019 |
| 4. | Mwongozo wa Kusimamia na Kuendesha Tovuti za Serikali | - | Desemba – 2014 |
| 5. | Mwongozo wa Mawasiliano kwa Njia ya Video Serikalini | - | Desemba – 2014 |
| 6. | Mwongozo wa Usimamizi wa Miradi ya TEHAMA | - | Toleo 1.0 Jan – 2010 |
| 7. | Mwongozo wa Matumizi Bora, Sahihi na Salama ya Vifaa na Mifumo ya TEHAMA Serikalini | - | 2022 |

## B. Miongozo ya Kiufundi – Ngazi ya 2

| Na | Jina la Nyaraka | Namba ya Nyaraka | Toleo & Mwaka |
|---|---|---|---|
| **1.** | **Usanifishaji wa Dira ya Serikali Mtandao – Viwango na Miongozo ya Kiufundi** | **eGA/EXT/AVS/001** | **Toleo 1.0 – Novemba 2017** |
| i. | Mwongozo wa Kiufundi wa Uandaaji Nyaraka ya Usimamizi wa TEHAMA | eGA/EXT/AVS/003 | Toleo 1.0 – Julai 2022 |
| ii. | Mwongozo wa Utendaji wa Kamati ya Uendeshaji wa TEHAMA kwa Taasisi | eGA/EXT/AVS/006 | Toleo 1.0 – Aprili 2020 |
| iii. | Mwongozo wa Hali ya Ukomavu wa Serikali Mtandao | eGA/EXT/AVS/007 | Toleo 1.0 – Mei 2023 |
| **2.** | **Usanifishaji Shughuli za Serikali Mtandao – Viwango na Miongozo ya Kiufundi** | **eGA/EXT/BSA/001** | **Toleo 1.0 – Novemba 2017** |
| i. | Taratibu za Serikali za Ugawaji wa Namba za Huduma za Serikali kwa Simu za Mkononi | eGA/EXT/PRC/001 | Rev 1.0 – Machi 2024 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| ii. | Vigezo na Orodha Hakiki ya Serikali ya Kupitia Miradi ya TEHAMA | eGA/EXT/BSA/11 | Toleo 1.0 – Desemba 2024 |
| | | eGA/EXT/PRC/004 | Toleo 1.0 – Agosti 2014 |
| iii. | Dawati la Huduma kwa Mteja na Mchakato wa Kusaidia TEHAMA | eGA/EXT/BSA/004 | Toleo 1.0 – Aprili 2016 |
| iv. | Miongozo ya majukumu ya kiusalama ya huduma za Mamlaka ya Serikali mtandao | eGA/EXT/BSA/005 | Toleo 1.0 – Julai 2019 |
| v. | Mfumo wa uendelevu wa huduma za kielekroniki | eGA/EXT/BSA/006 | Toleo 1.0 – Mei 2024 |
| vi. | Viwango na Miongozo ya Utekelezaji wa Miradi ya TEHAMA ya Serikali | eGA/EXT/BSA/008 | Toleo 1.0 – Desemba 2024 |
| vii. | Taratibu za Uidhinishaji, Ufuatiliaji na Ukamilishwaji wa Miradi ya TEHAMA ya Serikali | eGA/EXT/BSA/009 | Toleo 1.0 – Desemba 2024 |
| **3.** | **Usanifishaji wa Taarifa za Serikali Mtandao – Viwango na Miongozo ya Kiufundi** | **eGA/EXT/IFA/001** | **Toleo 1.0 – Novemba 2017** |
| i. | Viwango na Miongozo ya Kiufundi ya Kamusi ya Taarifa za Taasisi | eGA/EXT/IFA/002 | Toleo 1.0 – Julai 2021 |
| **4.** | **Usanifishaji wa Miundombinu ya Serikali Mtandao –Viwango na Miongozo ya Kiufundi** | **eGA/EXT/IRA/001** | **Toleo 1.0 – Novemba 2017** |
| i. | Mwongozo wa mawasiliano kwa njia ya Video Serikalini | eGA/EXT/IRA/002 | Toleo 1.0 – Aprili 2020 |
| ii. | Viwango vya Vituo vya Kuhifadhi Data kwa Taasisi za Umma | eGA/EXT/IRA/003 | Toleo 1.0 – Desemba 2020 |
| iii. | Viwango vya Vifaa na Programu za Serikali | eGA/EXT/IRA/004 | Toleo 1.0 – Julai 2022 |
| iv. | Sifa Mahususi za Vifaa na Programu za Serikali | eGA/EXT/IRA/005 | Toleo 2.0 – Februari 2024 |
| v. | Viwango na Miongozo ya Utayari wa TEHAMA katika Miundombinu Inayomilikiwa na Serikali | eGA/EXT/IRA/006 | Toleo 1.0 – Julai 2022 |
| vi. | Mwongozo na Vigezo vya kusimika Mifumo ya kujitegemea na mifumo ya pamoja ya Serikali | eGA/EXT/IRA/007 | Toleo 1.0 – Julai 2022 |
| vii. | Uelekeo wa Tekinologia katika Serikali Mtandao | eGA/EXT/IRA/008 | Toleo 1.0 – Februari 2024 |
| **5.** | **Usanifishaji Programu Tumizi za Serikali Mtandao – Viwango na Miongozo ya Kiufundi** | **eGA/EXT/APA/001** | **Toleo 1.0 – Novemba 2017** |
| i. | Orodha Hakika ya Ubora wa Mifumo Tumizi | eGA/EXT/APA/002 | Toleo 2.0 – Mei 2024 |
| ii. | Viwango vya Majina ya Anwani za Tovuti za Serikali | eGA/EXT/APA/003 | Toleo 2.1 – Julai 2022 |
| iii. | Viwango vya Majina ya Barua Pepe Serikalini | eGA/EXT/APA/004 | Toleo 1.0 – Julai 2022 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| iv. | Viwango vya Utengenezaji, Ununuzi, Undeshaji na Usimamizi wa Mifumo Tumizi ya Serikali Mtandao. | eGA/EXT/APA/005 | Toleo 2.0 – Julai 2022 |
| v. | Miongozo ya Utengenezaji, Ununuzi, Uendeshaji na Usimamizi wa Mifumo Tumizi ya Serikali Mtandao | eGA/EXT/APA/006 | Toleo 2.0 – Machi 2020 |
| vi. | Miongozo ya Ufuasi wa Uhakiki wa Ubora kwa Mifumo Tumizi ya Serikali Mtandao | eGA/EXT/APA/007 | Toleo 1.2 – Mei 2024 |
| vii. | Viwango vya kiufundi na Miongozo ya Tovuti ya Serikali | eGA/EXT/APA/009 | Toleo 2.0 – Julai 2022 |
| viii. | Orodha Hakiki na Ukaguzi wa Uingizaji Data | eGA/EXT/APA/010 | Toleo 1.1 Mei 2024 |
| **6.** | **Usanifishaji wa Usalama wa Serikali Mtandao – Viwango na Miongozo ya Kiufundi** | **eGA/EXT/ISA/001** | **Toleo 1.0 – Novemba 2017** |
| i. | Uandaaji Sera ya Usalama wa TEHAMA – Mwongozo wa Kiufundi | eGA/EXT/ISA/003 | Toleo 1.0 – Mei 2024 |
| ii. | Mwongozo wa Operesheni za Usalama wa Serikali Mtandao | eGA/EXT/ISA/004 | Toleo 1.0 – Agosti 2023 |
| **7.** | **Usanifishaji Utangamanishi wa Serikali Mtandao** | **eGA/EXT/ITA/001** | **Toleo 1.0 – Novemba 2017** |
| i. | Mwongozo ya Ubadilishanaji wa Taarifa za Kielektroniki | eGA/EXT/ITA/002 | Toleo 1.1 – Julai 2022 |
| ii. | Mwongozo wa ubadilishanaji Taarifa kupitia Mfumo wa Ubadilishanaji wa Taarifa Serikalini (GOVESB) | eGA/EXT/ITA/003 | Toleo 1.0 – Julai 2022 |
| **8.** | **Mchakato wa Serikali Mtandao na Usimamizi – Viwango na Miongozo ya Kiufundi** | **eGA/EXT/PAG/001** | **Toleo 1.0 – Novemba 2017** |
| **9.** | **Mfumo wa Serikali Mtandao Kuwasiliana – Viwango na Miongozo ya Kiufundi** | **eGA/EXT/GIF/001** | **Toleo 1.0 – Februari 2016** |

## C. Miongozo ya Kitaasisi – Ngazi ya 3

| Na | Jina la Nyaraka | Namba ya Nyaraka | Toleo & Mwaka |
|---|---|---|---|
| **1.** | Sampuli ya Sera ya TEHAMA | eGA/EXT/SAM/001 | Toleo 1.0 – Februari 2016 |
| **2.** | Sampuli ya Sera ya Usalama wa TEHAMA | eGA/EXT/SAM/002 | Toleo 1.0 – Februari 2016 |
| **3.** | Sampuli ya Sera ya Matumizi Rasmi ya TEHAMA | eGA/EXT/SAM/003 | Toleo 1.0 – Februari 2016 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **4.** | Kiolezo cha Ripoti ya Utekelezaji wa Serikali Mtandao | eGA/EXT/TEM/001 | Toleo 1.0 – Desemba 2020 |
| **5.** | Kiolezo cha Andiko la Mradi wa TEHAMA | eGA/EXT/TEM/002 | Toleo 1.0 – Desemba 2020 |
| **6.** | Kiolezo cha Pendekezo la Mradi wa TEHAMA | eGA/EXT/TEM/003 | Toleo 1.0 – Desemba 2020 |
| **7.** | Kiolezo cha Ripoti ya Maendeleo ya Mradi wa TEHAMA | eGA/EXT/TEM/004 | Toleo 1.0 – Desemba 2020 |
| **8.** | Kiolezo cha Ripoti ya Ukamilifu wa Mradi wa TEHAMA | eGA/EXT/TEM/005 | Toleo 1.0 – Desemba 2020 |
| **9.** | Sampuli ya Mpango Mkakati wa Kujihami na Majanga ya TEHAMA | eGA/EXT/SAM/004 | Toleo 1.0 – Septemba 2021 |
| **10.** | Sampuli ya Mpango Mkakati wa TEHAMA | eGA/EXT/SAM/005 | Toleo 1.0 – Septemba 2021 |
| **11.** | Sampuli ya Makubaliano ya Uendeshaji Huduma za TEHAMA | eGA/EXT/SAM/006 | Toleo 1.0 – Septemba 2021 |
| **12.** | Sampuli ya Taratibu za Usimamizi wa Huduma za TEHAMA | eGA/EXT/SAM/007 | Toleo 1.0 – Septemba 2021 |
| **13.** | Sampuli ya Nyaraka ya Taratibu za Utengenezaji, Ununuzi, Uendeshaji na Usimamizi wa TEHAMA | eGA/EXT/SAM/008 | Toleo 1.0 – Machi 2024 |

# 2. Maelezo ya Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao

## A. Miongozo ya Ngazi ya Sera – Ngazi ya 1

| KUNDI | JINA LA NYARAKA | MAELEZO |
|---|---|---|
| **Mwongozo wa Serikali Mtandao** | **Mwongozo wa Serikali Mtandao - 2017** | Huu ni mwongozo wa kiufundi kwa taasisi za umma na watumishi wa umma juu ya matumizi ya TEHAMA na vifaa vinavyohusiana na TEHAMA. |
| | **NYARAKA ZINAZOHUSIANA** | |
| | **Mwongozo wa Mawasiliano kwa Njia ya Video Serikalini.** | Mwongozo huu hutoa taratibu na majukumu ya kuzingatia kwa Taasisi za Umma na watumishi wa umma katika matumizi ya mawasiliano kwa njia ya mkutano wa video. |
| | **Mwongozo wa Kusimamia na Kuendesha Tovuti za Serikali** | Mwongozo huu ni maelekezo ya kiufundi kuhusu kusanifu, kuendesha na kuhifadhi tovuti za Serikali kwa mujibu wa viwango vinavyokubalika kimataifa. |
| | **Mwongozo na VIwango vya Mfumo Jumuishi wa Kielektroni wa Usimamizi wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya** | Mwongozo huu unaeleza masharti, viwango na miongozo kwa ajili ya utekelezaji wenye mfanikio na matumizi ya Mfumo Jumuishi wa Kielektroni wa Usimamizi wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya vya umma na vya binafsi nchini Tanzania. Pia unaeleza muundo wa uongozi na utawala katika Kamati ya |

| | | |
|---|---|---|
| | | Taifa ya Uendeshaji wa afya mtandao (NeHSC) utakao saidia kuhakikisha utekelezai wa jitihada za afya mtandao kwa wakati. |
| | **Mwongozo wa Usanifishaji Mpango wa Shughuli** | Nyaraka hii inaelezea hatua kwa hatua katika uundaji wa usanifu wa biashara ili kufikia uwiano wa biashara na TEHAMA katika shirika. |
| | **Mwongozo wa Usimamizi wa Miradi ya TEHAMA** | Mwongozo huu unaeleza mbinu ya hatua kwa hatua na kwa vitendo kwa ajili ya kuwezesha usimamizi wa Miradi kwa utekelezaji wenye ufanisi wa miradi ya TEHAMA na kudhibiti athari za utekelezaji. |
| | **Mwongozo wa Matumizi Bora, Sahihi na Salama ya Vifaa na Mifumo ya TEHAMA Serikalini** | Mwongozo huu unatoa maelekezo na taratibu zinazotakiwa kufuatwa na watumishi wa Umma katika matumizi mbalimbali ya TEHAMA na vifaa vinavyohusiana na teknolojia hiyo. |

## B. Miongozo ya Kiufundi – Ngazi ya 2

| KUNDI | JINA LA NYARAKA | MAELEZO |
|---|---|---|
| **Usanifishaji wa Dira ya Serikali Mtandao** | **Usanifishaji wa Dira ya Serikali Mtandao – Viwango na Miongozo ya Kiufundi** | Inatoa maelezo yanayohusiana na serikali nzima, huduma za serikali, data, program tumizi na modeli rejea za teknolojia zinafafanuliwa. |
| | **NYARAKA ZINAZOHUSIANA** | |
| | **Uandaaji Nyaraka ya Usimamizi wa TEHAMA – Mwongozo wa Kiufundi** | Mwongozo wa kuandaa Nyaraka za usimamizi wa TEHAMA Serikalini. |
| | **Mwongozo wa Utendaji wa Kamati ya Uendeshaji wa TEHAMA kwa Taasisi** | Miongozo hii inatoa maelekezo kuhusu namna Mwongozo wa Utendaji wa Kamati ya Uendeshaji wa TEHAMA kwa Taasisi itakavyoendeshwa kwenye sekta ya umma kwa kueleza maudhui ya waraka wa kamati unaotamka masharti ya marejeo. |
| | **Mwongozo wa Hali ya Ukomavu wa Serikali Mtandao** | Mwongozo huu unatoa namna na zana kwa Taasisi ya Umma kufanya tathmini binafsi za kubaini hali zao za ukomavu wa TEHAMA. |
| **Mfumo wa Serikali Mtandao Kuwasiliana** | **Mfumo wa Serikali Mtandao Kuwasiliana – Viwango na Miongozo ya Kiufundi** | Hutoa taarifa kwa serikali kuhusu kubadilishana, kushirikiana na kujumuisha taarifa na kupanga michakato yake kwa kutumia viwango vya wazi vya kawaida. |
| **Usanifishaji Shughuli za** | **Usanifishaji Shughuli za Serikali Mtandao – Viwango na Miongozo ya Kiufundi** | Hutoa maelezo yanayohusiana na utoaji wa |

| | | |
|---|---|---|
| **Serikali Mtandao** | | huduma za Serikali zilizo muhimu, nyumbufu na nyeti kwa mahitaji ya wananchi pamoja na huduma za kawaida zinazoweza kutumiwa tena na taasisi nyingine za umma. |
| | **NYARAKA ZINAZOHUSIANA** | |
| | **Taratibu za Serikali za Ugawaji wa Namba za Huduma za Serikali kwa Simu za Mkononi** | Nyaraka hii inatoa masharti na taratibu zitakazofuatwa na taasisi za umma kwa ugawaji wa namba za huduma za Serikali kwa simu za mkononi. |
| | **Vigezo na orodha ya kuhakiki miradi ya TEHAMA** | Nyaraka hii inaelezea vigezo vya kupitia miradi ya TEHAMA kwa lengo la kutoa njia iliyo wazi, yenye lengo maalum, na thabiti katika utoaji wa idhini na mapendekezo ya kiufundi kwa miradi ya TEHAMA inayowasilishwa. Zaidi ya hayo, pia inatoa orodha ya ukaguzi ambayo Taasisi za Umma zinapaswa kutumia kwa kujitathmini kabla ya kuwasilisha mradi wa TEHAMA kwa Mamlaka. |
| | **Dawati la Huduma kwa Mteja na Mchakato wa Kusaidia TEHAMA** | Nyaraka hii inaeleza namna Dawati la Huduma kwa Mteja la Serikali Mtandao na Michakato ya kusaidia TEHAMA inavyoanzishwa, kusimamiwa, kuripotiwa na kutengenezwa na e-GA kwa ajili ya Taasisi za Umma. |

| | | |
|---|---|---|
| | **Miongozo ya majukumu ya kiusalama ya huduma za Mamlaka ya Serikali mtandao** | Nyaraka hii inaweka bayana mgawanyo wa majukumu ya usalama wa TEHAMA kati ya mpokeaji wa huduma (Taasisi ya Umma) na mtoaji wa huduma (e-GA) katika kipindi chote cha utoaji huduma ya Serikali mtandao. |
| | **Mfumo wa uendelevu wa huduma za kielekroniki** | Nyaraka hii ni kuhakikisha kuwa Huduma za kielekroniki ni endelevu na zinatimiza malengo ya Taasisi za Umma kwa kutoa huduma endelevu zinazoendana na Viwango na Miongozo ya Serikali mtandao. |
| | **Viwango na Miongozo ya Utekelezaji wa Miradi ya TEHAMA ya Serikali** | Hutoa Mwongozo kwa Taasisi za Umma katika kusimamia miradi ya TEHAMA ili kuhakikisha inatekelezwa kwa ufanisi, isio endeshwa na mkandarasi, isiyo jirudia, manufaa yanapatikana na rasilimali zinaboreshwa. |
| | **Taratibu za Uidhinishaji, Ufuatiliaji na Ukamilishwaji wa Miradi ya TEHAMA ya Serikali** | Inaeleza taratibu za Mamlaka ya Serikali katika kutekeleza kwa ufanisi uidhinishaji, ufuatiliaji na udhibiti wa miradi ya Serikali Mtandao, pamoja na kuhakikisha inakamilishwa. |
| **Usanifishaji Programu Tumizi za Serikali Mtandao** | **Usanifishaji Programu Tumizi za Serikali Mtandao – Viwango na Miongozo ya Kiufundi** | Hutoa taarifa kuhusu usanifishaji mfumo tumizi katika Serikali. Usanifishaji huu unajumuisha maeneo ya utumikaji na urahisi, yanayolenga huduma, uzingatiaji wa viwango vya wazi, utumikaji tena, urahisi |

| | | |
|---|---|---|
| | | wa kubadilika kulingana na hali na kutumika maeneo mengine mbalimabali. |
| | **NYARAKA ZINAZOHUSIANA** | |
| | **Viwango vya Majina ya Anwani za Tovuti za Serikali** | Nyaraka hii inaviwango vya kuandika majina ya anuani za Tovuti za Serikali Tanzania na kuonesha uchaguzi walazima na hiari uliopo katika kuandika majina ya anuani ya tovuti za Serikali. |
| | **Viwango vya Majina ya Barua Pepe Serikalini** | Nyaraka hii ina utaratibu wa kiwango cha kusimamia akaunti za baruapepe kwenye Taasisi za Umma kama vile majina, uandikaji, marekebisho n.k. |
| | **Orodha Hakiki na Ukaguzi wa Uingizaji Data** | Orodha hakiki hii imesanifiwa kusaidia kutathimini michakato na taratibu zinazotumika kufuatilia na kuripoti kuhusu michakato ya uingizaji data na uhifadhi. |
| | **Orodha Hakika ya Ubora wa Mifumo Tumizi** | Orodha hakiki hii itasaidi kuhakikisha uhakiki wa ubora wenye ufanisi na unaofaa wa michakato katika utaratibu wa utengenezaji wa mifumo tumizi. |
| | **Miongozo ya Utengenezaji, Ununuzi, Uendeshaji na Usimamizi wa Mifumo Tumizi ya Serikali Mtandao** | Nyaraka hii inaweka Miongozo ya utengenezaji, ununuzi, uendeshaji na usimamizi wa mifumo inayotumiwa na taasisi za umma kwa ajili ya shughuli za serikali mtandao. |

| | | |
|---|---|---|
| | **Miongozo ya Ufuasi wa Uhakiki wa Ubora kwa Mifumo Tumizi ya Serikali Mtandao** | Miongozo ya Ufuasi wa Uhakiki wa Ubora kwa Mifumo Tumizi ya Serikali Mtandao inaeleza njia ambazo Taasisi za Serikali au wakaguzi/ wakadiriaji watatumia kuhakiki ufuasi wa Mifumo Tumizi ya Serikali Mtandao kwa masharti ya ubora. |
| | **Viwango vya Utengenezaji, Ununuzi, Undeshaji na Usimamizi wa Mifumo Tumizi ya Serikali Mtandao** | Viwango vya mifumo tumizi, utengenezaji, undeshaji na usimamizi hueleza kwa kina hatua zitakazosaidia Taasisi za Umma kutoa uamuzi iwapo kutengeneza mifumo ndani ya taasisi, kununua au kukodi mifumo tumizi na namna ya kusimamia mifumo hiyo. |
| | **Viwango vya kiufundi na Miongozo ya Tovuti ya Serikali** | Hati hii inatoa Viwango na Miongozo ya kiufundi ya kuunda tovuti za Serikali zinazokidhi vigezo vya watumiaji kama vile urahisi wa kutumia na ufikivu. |
| **Usanifishaji wa Taarifa za Serikali Mtandao** | **Usanifishaji wa Taarifa za Serikali Mtandao – Viwango na Miongozo ya Kiufundi** | Hufafanua maagizo ya usanifishaji wa taarifa kwa ajili ya ukusanyaji wa data, upatikanaji, umiliki, usalama na usiri, uhifadhi na utunzaji, ufafanuzi na viwango vya matumizi ya data za kawaida na metadata. |
| | **NYARAKA ZINAZOHUSIANA** | |
| | **Viwango na Miongozo ya Kiufundi ya Kamusi ya Taarifa za Taasisi** | Inaelezea Viwango na Miongozo ya kufuatwa wakati wa utayarishaji wa kamusi ya data ya Taasisi kulingana na kifungu namba 54 cha |

| | | |
|---|---|---|
| | | Kanuni za Serikali Mtandao ya mwaka, 2020. |
| **Usanifishaji Utangamanishi wa Serikali Mtandao** | **Usanifishaji Utangamanishi wa Serikali Mtandao** | Hutoa maelezo ya usanifishaji utangamanishi kwa namna kuwa program tumizi mbalimbali za taasisi za umma zinatangamanishwa kuwezesha ubadilishanaji taarifa ndani ya serikali. |
| | **NYARAKA ZINAZOHUSIANA** | |
| | **Miongozo ya Ubadilishanaji wa Taarifa za Kielektroniki** | Hutoa Mwongozo wa kubadilishana data za kielektroniki baina ya Taasisi za Umma. |
| | **Mwongozo wa ubadilishanaji Taarifa kupitia Mfumo wa Ubadilishanaji wa Taarifa Serikalini (GOVESB)** | Mwongozo huu unaanisha vigezo vya kuwezesha ubadilishanaji wa data kwa mifumo ya Taasisi za Umma kwa kupitia Mfumo wa Ubadilishanaji wa Taarifa Serikalini (GovESB) |
| **Usanifishaji wa Miundombinu ya Serikali Mtandao** | **Usanifishaji wa Miundombinu ya Serikali Mtandao –Viwango na Miongozo ya Kiufundi** | Hutoa taarifa za miundombinu ya teknolojia inayosaidia shughuli za Serikali kama vile seva, kituo cha kazi, uhifadhi na miundombinu ya mtandao, utoaji leseni wa program za kompyuta, kukabili majanga ya TEHAMA na uendelevu wa shughuli, usimamizi wa mtoa huduma za TEHAMA, vipengele vya usimamizi wa rasilimali watu na huduma. |
| | **NYARAKA ZINAZOHUSIANA** | |
| | **Mwongozo wa mawasiliano kwa njia ya Video Serikalini** | Unaeleza masharti na kanuni zitakazotumika kwa ajili ya |

| | | |
|---|---|---|
| | | utekelezaji wa uendeshaji mikutano kwa njia ya video Serikalini |
| | **Viwango vya Vituo vya Kuhifadhi Data kwa Taasisi za Umma** | Mwongozo kwa Taasisi za Umma Katika kuchagua mahali sahihi pa kuhifadhi data, na sio kujenga kituo kipya. Pia, Viwango hivyo vitatumika kama mahitaji ya chini katika kutathmini ubora wa kituo, na kuidhinishwa kama mahali sahihi pa kuhifadhi data. |
| | **Viwango vya Vifaa na Programu za Serikali** | Nyaraka hii inaweka bayana mahitaji ya chini ya vifaa na programu za TEHAMA zinazopaswa kutumika katika Taasisi za Umma. |
| | **Sifa Mahususi za Vifaa na Programu za Serikali** | Hutoa sifa mahususi za vifaa na programu za TEHAMA kwa madhumuni ya matumizi sahihi na usimamizi wa rasilimali za TEHAMA zinazomilikiwa na Serikali. |
| | **Viwango na Miongozo ya Utayari wa TEHAMA katika Miundombinu Inayomilikiwa na Serikali** | Nyaraka hii inatoa viwango, na miongozo ya kiufundi kuhakikisha utayari wa TEHAMA wakati wa kujenga miundombinu yoyote inayomilikiwa na Serikali kama vile barabara, madaraja, reli na majengo. |
| | **Mwongozo na Vigezo vya kusimika Mifumo ya kujitegemea na mifumo ya pamoja ya Serikali** | Nyaraka hii inatoa mwongozo na vigezo kwa Taasisi za Umma vya kuchagua kutumia mifumo ya kujitegemea au mifumo ya pamoja ya Serikali. |

| | | |
|---|---|---|
| | **Uelekeo wa Tekinologia katika Serikali Mtandao** | Nyaraka hii inatoa uelekeo wa utumiaji wa tekinologia mbalimbali katika utekelezaji wa Serikali Mtandao. |
| **Usanifishaji wa Usalama wa Serikali Mtandao** | **Usanifishaji wa Usalama wa Serikali Mtandao – Viwango na Miongozo ya Kiufundi** | Hutoa taarifa ya namna ya kukinga na kulinda kiiktisadi taasisi za umma kutokana na matishio ya kiusalama wakati huo huo na kufuata masharti ya kiusalama na kisheria kwa ajili ya usiri, faragha, ufikiwaji, upatikanaji na uadilifu. |
| | **NYARAKA ZINAZOHUSIANA** | |
| | **Uandaaji Sera ya Usalama wa TEHAMA – Mwongozo wa Kiufundi** | Mwongozo wa jinsi ya kuandaa sera ya Usalama wa TEHAMA ya taasisi. |
| | **Mwongozo wa Operesheni za Usalama wa Serikali Mtandao** | Nyaraka hii inatoa Miongozo ya operesheni na utekelezaji wa shughuli za usalama wa Serikali Mtandao kwa Taasisi za Umma. |
| **Mchakato wa Serikali Mtandao na Usimamizi** | **Mchakato wa Serikali Mtandao na Usimamizi – Viwango na Miongozo ya Kiufundi** | Mwongozo huainisha seti ya mapendekezo ya taratibu za usimamizi ambao viwango na miongozo inayohusiana na serikali mtandao hupitia kutoka ngazi ya taifa na kuchukuliwa na kutekelezwa ngazi ya taasisi ya umma. |

## C. Miongozo ya Kitaasisi – Ngazi ya 3

| KUNDI | JINA LA NYARAKA | MAELEZO |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| **Sera ya TEHAMA** | **Sampuli ya Sera ya TEHAMA** | Mwongozo wa jinsi ya kuandaa sera ya TEHAMA katika taasisi za Serikali. |
| | **NYARAKA ZINAZOHUSIANA** | |
| | **Sampuli ya Mpango Mkakati wa TEHAMA** | Sampuli ambayo inaweza kutumiwa na taasisi za umma katika uandaaji wa Mpango Mkakati wa TEHAMA. |
| **Sera ya Usalama wa TEHAMA** | **Sampuli ya Sera ya Usalama wa TEHAMA** | Sampuli ambayo inaweza kutumiwa na taasisi za umma katika uandaaji wa sera ya Usalama wa TEHAMA. |
| | **NYARAKA ZINAZOHUSIANA** | |
| | **Mpango Mkakati wa Kujihami na Majanga ya TEHAMA** | Sampuli ambayo inaweza kutumiwa na taasisi za umma katika uandaaji wa Mpango Mkakati wa Kujihami na Majanga ya TEHAMA. |
| **Sera Rasmi ya Matumizi ya TEHAMA** | **Sampuli ya Sera ya Matumizi Rasmi ya TEHAMA** | Mwongozo wa kuandaa sera ya kusimamia matumizi rasmi ya TEHAMA ndani ya taasisi. |
| **Kiolezo cha Ripoti ya Utekelezaji wa Serikali Mtandao** | **Kiolezo cha Ripoti ya Utekelezaji wa Serikali Mtandao** | Kiolezo ambacho kinaweza kutumiwa na taasisi za umma katika uandaaji wa Ripoti ya Utekelezaji wa Serikali Mtandao. |
| | **NYARAKA ZINAZOHUSIANA** | |
| | **Kiolezo cha Andiko la Mradi wa TEHAMA** | Kiolezo ambacho kinaweza kutumiwa na taasisi za umma katika uandaaji wa Andiko la Mradi wa TEHAMA. |
| | **Kiolezo cha Pendekezo la Mradi wa TEHAMA** | Kiolezo ambacho kinaweza kutumiwa na taasisi za umma katika uandaaji wa Pendekezo la Mradi wa TEHAMA. |

| | | |
|---|---|---|
| | **Kiolezo cha Ripoti ya Maendeleo ya Mradi wa TEHAMA** | Kiolezo ambacho kinaweza kutumiwa na taasisi za umma katika uandaaji wa Ripoti ya Maendeleo ya Mradi wa TEHAMA. |
| | **Kiolezo cha Ripoti ya Ukamilifu wa Mradi wa TEHAMA** | Kiolezo ambacho kinaweza kutumiwa na taasisi za umma katika uandaaji wa Ripoti ya Ukamilifu wa Mradi wa TEHAMA. |
| **Sampuli ya Taratibu za Usimamizi wa Huduma za TEHAMA** | **Sampuli ya Taratibu za Usimamizi wa Huduma za TEHAMA** | Sampuli ambayo inaweza kutumiwa na taasisi za umma katika uandaaji wa Taratibu za Usimamizi wa Huduma za TEHAMA. |
| | **NYARAKA ZINAZOHUSIANA** | |
| | **Sampuli ya Makubaliano ya Uendeshaji Huduma za TEHAMA** | Sampuli ambayo inaweza kutumiwa na taasisi za umma katika uandaaji wa Makubaliano ya Uendeshaji Huduma za TEHAMA. |
| **Sampuli ya Nyaraka ya Taratibu za Utengenezaji, Ununuzi, Uendeshaji na Usimamizi wa TEHAMA** | **Sampuli ya Nyaraka ya Taratibu za Utengenezaji, Ununuzi, Uendeshaji na Usimamizi wa TEHAMA** | Sampuli ambayo inaweza kutumiwa na taasisi za umma katika uandaaji wa Taratibu za Utengenezaji, Ununuzi, Uendeshaji na Usimamizi wa TEHAMA. |

# 3. Maelezo ya Nyaraka Zinazohusiana


## Sheria, Sera, Miongozo na Mikakati mbalimbali ya Serikali Mtandao

| AINA | JINA LA NYARAKA | MAELEZO |
|---|---|---|
| **Sera** | **Serikali**<br><br>**Sera ya Taifa ya TEHAMA 2016** | Sera ya Taifa ya TEHAMA 2016 (NICTP 2016), ambayo ni matokeo ya marekebisho ya NICTP 2003 inatoa mfumo kamili wa kuongoza maendeleo na ukuaji wa sekta ya TEHAMA ili kuhakikisha faida kwa taifa na raia wake. |
| **Sheria** | **Serikali**<br><br>**Sheria ya Serikali Mtandao, 2019** | Sheria ya huduma za Serikali Mtandao; Uanzishwaji wa Mamlaka ya Serikali Mtandao na utawala wake; Usimamizi na uendeshaji wa huduma za Serikali Mtandao; Usimamizi wa data za kielektroniki na mambo mengine yanayohusiana. |
| | **Sheria ya Mawasiliano ya Posta na Kielekroni 2010**<br><br>**Marekebisho ya Sheria ya Mawasiliano ya Posta na Kielekroni 2010** | Sheria ya mawasiliano ya kielektroniki na posta, kwa mtazamo wa kuzingatia maendeleo katika sekta ya mawasiliano ya kielektroniki. |
| | **Sheria ya Makosa ya Kimtandao, 2015** | Sheria ya makosa ya jinai kuhusiana na mifumo ya kompyuta na Teknolojia ya Habari za Mawasiliano, kwa ajili ya uchunguzi, kukusanya, na matumizi ya ushahidi wa elektroniki na mambo yanayohusiana. |
| | **Sheria ya Miamala ya Kielekroni 2015** | Sheria hii inatoa utambuzi wa kisheria wa huduma za |

| | | |
|---|---|---|
| | | kielektroniki, huduma za Serikali Mtandao, na matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika ukusanyaji wa ushahidi, kukubalika kwa ushahidi wa kielektroniki na kuwezesha matumizi salama ya saini za kielekroniki. |
| **Kanuni** | **Serikali**<br><br>**Kanuni ya Serikali Mtandao, 2020** | Kanuni katika Usimamizi na Utendaji wa Serikali Mtandao; Miundombinu na Mifumo ya Serikali Mtandao; Huduma za Serikali Mtandao; Usalama wa Serikali Mtandao; Usimamizi wa data za kielectroniki za Serikali na mambo mengine yanayohusiana. |
| | Kanuni za Timu ya Dharura ya Mifumo ya Kompyuta (CERT) | Hizi ni kanuni kwa timu inayohusika na matukio ya usalama wa kompyuta, katika kutoa huduma muhimu ili kutatua na kuzuia matukio yoyote ya usalama wa kompyuta, kwa waendeshaji wote wa mawasiliano ya kielektroniki, watoa huduma za mtandao na watumiaji. |
| **Waraka** | **Serikali**<br><br>Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na.3 wa Mwaka 2013 | Waraka unaotoa mwongozo wa Serikali katika matumizi mbalimbali ya TEHNOHAMA na vifaa vinavyohusiana na teknolojia hiyo katika ofisi za Serikali. |
| | Waraka wa Utumishi Na.5 wa Vifaa vya Teknohama Serikalini | Waraka unaotoa mwongozo wa Serikali katika matumizi mbalimbali ya TEHNOHAMA na vifaa vinavyohusiana na |

| | | |
|---|---|---|
| | | teknolojia hiyo katika ofisi za Serikali. |
| **Mikakati** | **Serikali**<br><br>[Mkakati wa Serikali Mtandao Tanzania] | Mkakati huu hutoa mwongozo kwa raia kuhusiana na mipango ya Serikali Mtandao Tanzania, kuhakikisha inaleta huduma karibu na wananchi kwa kutumia zaidi Teknologia ya Habari na Mawasiliano. |
| | **Sekta**<br><br>[Mkakati wa Afya wa Kidijitali Tanzania 2019-2024] | Mkakati wa Afya wa Kidijitali 2019-2024 unaoelezea maono ya muda mrefu ya Afya ya Kidigitali Tanzania, na kuzingatia juu ya faida zitakazotolewa kwa miaka mitano ijayo. Lengo kuu la Mkakati huu ni kusaidia katika mageuzi ya mfumo wa afya wa Tanzania kwa kutumia teknolojia, matumizi ya data, na kuzingatia mahitaji halisi ya mteja wa afya na jumuishi ili kuboresha upatikanaji na ubora wa huduma za afya kwa Watanzania wote; inaangazia uboreshaji wa teknolojia za kidijitali ili kufikia huduma ya afya kwa wote na kupatana na dira ya maendeleo ya 2025 ya nchi. |

# 4. Muundo wa Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao



# Maelezo ya Muundo wa Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao

Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao vina lengo la kusaidia Serikali katika utoaji wa huduma zilizothabiti zaidi na kutosheleza kwa wananchi na kusaidia utoaji wa huduma za TEHAMA unaozingatia thamani ya fedha na kutoa muundo ambao:

- Unasaidia kubainisha huduma rudufu, kutumika tena na kushirikiana;
- Unatoa msingi wa kutathmini uwekezaji wa Serikali katika TEHAMA, na
- Unawezesha utoaji kwa ufanisi zaidi wa huduma zilizo na gharama nafuu kutokana na kuwepo kwa viwango, kanuni na violezo vinavyosaidia katika kubuni na kutoa huduma za TEHAMA.

Muundo wa Viwango na Miongozo wa Serikali Mtandao umebuniwa kutosheleza mahitaji ya "Usanifishaji Shughuli Serikali Mtandao". Kwa maana hiyo Usanifishaji Shughuli Serikali Mtandao umo ndani ya "Viwango na Kanuni za Serikali Mtandao". Rejea rasmi za hali ya juu za Usanifishaji Shughuli Serikali Mtandao zipo kwenye nyaraka mama na nyaraka zinazohusiana hutoa maelezo ya kina kama yalivyotayarishwa na sekta na taasisi zenye Dira na Mifumo Mkakati.

- **Usanifishaji Shughuli Serikali Mtandao** - Kanuni zinazokubalika kimataifa kwa utekelezaji wa uchambuzi wa Serikali Mtandao, ubunifu, mipango na utekelezaji kwa kutumia mkabala ulio mpana wakati wote kwa maendeleo fanisi na utekelezaji wa Mkakati wa Serikali Mtandao.

## Aina za Nyaraka

**Ngazi ya Kwanza** – Ni Nyaraka za Miongozo ya Serikali Mtandao zinazotolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora kwa taasisi zote za Umma. Miongozo ya Serikali Mtandao ya kisekta - kwa mfano Afya-mtandao, Elimu-mtandao, Sheria-mtandao nk. Inayotolewa na Wizara iko katika kundi hili. Kuna waraka mama mmoja na nyaraka zinazohusiana zinazotoa miongozo ya Serikali ya Ngazi ya Sera kuhusu mambo ya Serikali Mtandao.

**Ngazi ya Pili** – Ni nyaraka za Viwango vya Kiufundi na Miongozo ya Serikali Mtandao zinazotolewa na Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa Taasisi za Umma kutoa "Viwango vya Serikali vya aina moja kuhusu utekelezaji wa Serikali Mtandao" na kutoa "Miongozo ya kiufundi ya namna ya kutekeleza jitihada za Serikali Mtandao". Nyaraka hizi hutumiwa zaidi na taasisi za umma wakati zinapotekeleza jitihada za Serikali Mtandao zenye maslahi kwa taifa, au zinazohitaji mawasiliano na zaidi ya taasisi moja. Nyaraka mama hutoa maelekezo rasmi na nyaraka zinazohusiana hujumuisha maoni ya kisekta na kitaasisi.

**Ngazi ya Tatu** – Ni nyaraka za TEHAMA kwa mfano Sera, Mwongozo, Mchakato, Taratibu na kadhalika, zinazotolewa na taasisi za umma kwa matumizi yao ya ndani. (Nyaraka hizi zinajulikana kuwa ni nyaraka za TEHAMA za Taasisi tofauti na za Ngazi ya Pili zinazojulikana kuwa ni nyaraka za TEHAMA za Serikali). Nyaraka za mifano zinazotayarishwa kusaidia Taasisi za Umma kuandaa nyaraka zao za Sera za TEHAMA au miongozo, pia hujulikana kuwa ni nyaraka za Ngazi ya Tatu.

# 5. Kanuni za Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao



## Maelezo ya Kanuni za Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao

| Kanuni | Sababu | Hatua za Kufuata |
|---|---|---|
| **1**. Serikali inalenga wananchi wake. | Serikali ipo kuhudumia umma wa watanzania wanaotaka kupata huduma na taarifa kwa urahisi, haraka na zilizo nafuu. | ▪ Taasisi za umma zitabuni na kutumia michakato ya shughuli na huduma zao kunufaisha wananchi, hata kama huduma hizo zitavuka mipaka ya shughuli zake.<br>▪ Serikali hutoa huduma iliyo sawa, ikipunguza urudufu, utata usio wa lazima na njia zisizotofautiana.<br>▪ Wananchi wanaweza kupata huduma za serikali kwa kutumia njia mbalimbali. |
| **2**. Serikali ni taasisi moja iliyoungana. | Shughuli moja yenye malengo mkakati shirikishi, utawala wa pamoja, michakato ya usimamizi iliyofungamanishwa na sera thabiti huboresha utekelezaji mikakati na uratibu wa utoaji huduma za serikali kwa wananchi. | ▪ Serikali inatenga rasilimali zake ili kutimiza malengo iliyojiwekea.<br>▪ Serikali inatumia taarifa kwa ukamilifu kwenye shughuli zote ili kusaidia huduma na michakato.<br>▪ Mipango iliyobuniwa hufungamanisha huduma kwa ajili ya kuleta ufanisi na kutoa uhuru wa utendaji wa shughuli kwa ajili ya kuleta mafanikio. |

| | | |
|---|---|---|
| | | ▪ Mipango iliyobuniwa hubainisha na kuruhusu mikabala ya kipekee kudumisha malengo muhimu ya sera. |
| **3**. Mfumo wa Serikali unatokana na dhamira mahususi. | Muundo unaozingatia shughuli hufanikiwa zaidi katika kutumiza malengo ya kimkakati kukidhi mahitaji ya mabadiliko ya dhamira na kuhudumia matarajio ya wananchi. | Muundo wa shughuli uliothibitishwa ni sharti muhimu la uwekezaji, kwa hiyo Wakuu wa Teknolojia ya Habari na watayarishaji mipango ni lazima washauriane na viongozi wa program ili waseme namna itakavyokuwa na kufanya kazi. Muundo huo unategemea zaidi mahitaji ya dhamira ya program na teknolojia wezeshi.<br><br>Taasisi za umma zitatumia kwanza kikamilifu michakato ya shughuli na halafu viwango vya utendaji kubainisha mahitaji ya uendeshaji.<br><br>Mifumo na michakato itatumia muundo ambao utashughulikia kwa haraka matukio, ikiwemo mbinu za kufikisha taarifa kwa watu wengi wakati mmoja.<br><br>Taasisi za umma zitatumia miundo ya taasisi zao kuongoza utayarishaji wa mipango ya maendeleo, bajeti na uamuzi wa uwekezaji. |

| | | |
|---|---|---|
| | | Taasisi za umma zitasimamia mabadiliko ya shughuli za Serikali kwa kuzingatia usalama wa kutosha kuwezesha huduma kuendelea.<br><br>Teknolojia ya habari serikalini lazima iweze kubadilika kulingana na mahitaji ya shughuli |
| **4**. Usalama, faragha na kulinda taarifa ni mahitaji ya msingi ya Serikali | Serikali lazina ilinde taarifa zake za siri ili kuongeza Imani ya wananchi na kuboresha usalama wa rasilimali zake. | ▪ Muktadha wa shughuli unaainisha mahitaji ya usalama na faragha, unaojumuishwa katika muundo wakati wa kipindi chote cha shughuli.<br>▪ Miundo ni lazima ionyeshe sera ili kupunguza matumizi mabaya ya data na ukiukaji wa usalama.<br>▪ Serikali ni lazima itumie viwango vya usalama na faragha wakti wote na kufuatilia utimizaji.<br>▪ Kanuni za usalama wa taarifa ni lazima ziwekwe wazi ili kuwianisha na kudhibiti gharama na vihatarishi |
| **5**. Taarifa ni rasilimali ya Taifa. | Wananchi arifu ni muhimu kwa demokrasia. Aidha taarifa sahihi ni muhimu katika utoaji uamuzi wenye tija, utendaji bora na utoaji sahihi wa taarifa. | ▪ Serikali itaboresha mazingira ya upashanaji taarifa ili kusambaza vizuri zaidi taarifa kwa umma.<br>▪ Hii inahitaji kubainisha vyanzo |

| | | |
|---|---|---|
| | | vyenye mamlaka ya taarifa za ubora wa hali ya juu na taasisi za umma kuruhusu upataji wa data na taarifa mahususi.<br>▪ Vyanzo vya data vyenye mamlaka ni lazima viundwe upya na kuorodheshwa kwa ajili ya usambazaji, upataji na usimamizi rahisi.<br>▪ Kutimiza kanuni hii kunahitajika mkakati wa serikali kuhamasisha uenezaji data wa gharama nafuu ndani na kwenye taasisi zote. |
| **6**. Muundo unarahisisha utendaji wa Serikali. | Mifumo na michakato tata yenye moduli zilizounganishwa ni migumu kusimamia, rahisi kushindwa, haibadiliki kuendana na mahitaji ya dhamira ya Mamlaka na ni ghali kuendesha. Mifumo ya moduli nyingi na michakato isiyounganishwa hunufaishwa na huduma shirikishi na mifumo inayotumika tena ndani ya serikali na kupatikana kibiashara. | ▪ Hii inahitaji mifumo tumizi isiyounganishwa inayotumiwa kama huduma na uendelezaji wa program zinazopatana.<br>▪ Taasisi za umma ni lazima zishirikiane mienendo bora na mifumo ya shughuli na ya kiufundi inayotumika tena.<br>▪ Kuunda na kujumuisha mifumo inayotumika tena ni lazima iwe ni njia ya kawaida ya uendelezaji. |